CHIFU TUMBO MBELE: Aha, mimi ni chifu mkuu Tumbo mbele, macho na maskio ya mfalme, aminiwe na mfalme. Mimi huhamasisha, kupanga na kutayarishamikutano mikuu kama hiyo ya mfalme.

Jioni njema, na sasa namwalika mfalme amatat, mtawala wan chi yetu.

(Umati Wanampokea kwa shangwe mfalme Matata Anainua mkono kuashiria watulie)

(Mfalme anasima na kuuhutubia umma)

MFALME MATATA: yezayeza

UMMATI: Yeba!

MFALME MATATA: Yeba Yeba!

UMMATI: Yeza!

MFALME MATATA: Wazee wa ufalme wa Kwetu, nawakaribisha kwenye kasri langu. Sina mengi ya kusema ila nawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkifanya katika ufalme wangu. Na sasa kwa uwezo na nguvu nilizopewa na mababu zetu ningependa kufungua rasmi msimu wa sherehe za tohara kama mojawapo ya tamaduni zetu. Kumbukeni watu bila tamaduni?

UMMATI: *(kwa sauti kubwa)* Ni watumwa

MFALME MATATA: YezaYeza!

UMMATI: Yeba!

CHIFU 1: Mfalme, wanaume, wanawake, wavulana na wasichana wako na furaha na tayari wanasubiri sherehe hizi. Nakuhakikishia mfalme wangu, kila kitu ki shwari kwa sherehe.

CHIFU 1: YebaYeba

UMMATI: Yeza!

BI KIZEE: Mfalme na wazee wenzangu kutoka ufalme mkuu wa kwetu, wacha tufurahi na tucheze densi kwa kuwa ni wakati wa kiwavi kukua na kuwa kipepeo. Wasichana wako tayari na kisu kimenolewa. Ni heshima kubwa kwangu kutekeleza wajibu wangu kwako tena musimu huu. Nakuomba wewe na mizimu ya mababu zetu iniongoze. Asante. kwako tena musimu huu. Nakuomba wewe na mizimu ya mababu zetu iniongoze. Asante.

MSIMULIZI: Wakati Bi Kizee anarudi kwenye kiti chake, umati unanong'onezana naye Bi. Faraja anainuka kuzungumza.

BI FARAJA (NAIBU WA CHIFU): Samahani mtukufu mfalme, nasema asante Sana kwa kuwa mmoja wa watu watakaoshuhudia sherehe za musimu huu. Lakini nina jambo ambalo linanisumbua roho kuhusu wasichana ambao tunataka kuwakomaza. Tumekuwa tukiwapoteza wasichana wetu, malaika wetu. Kwenye Sherehe za musimu uliopita msichana mmoja alivuja damu zaidi ya kawaida akaaga dunia na mwengine bado tunamuuguza, angali katika hali mahututi. Na hili swala bado hatujalitaua.

Mfalme pamoja na baadhi ya wazee tumechukua wakati na kusikiliza maoni ya wasicha na wanawake na pia wanaume wachache ambao wana wasiwasi kuhusu mateso ya kimwili na kiakili ambayo wasichana wetu wanapitia baada ya kukeketwa.

Wanaogopa kuzungumzia hadharani Kwa madai kwamba huenda wakabaguliwa, Mfalme wangu sauti zao hazisikiki wala kuheshimiwa

CHIFU TUMBO MBELE: Mtukufu mfalme, maneno ya Bi. Faraja ni tusi kwa tamaduni zetu na yanakera sana masikio ya mababu zetu. Hamna mtu anayetaka wala kuomba kifo kutokea, na kinapotokea ni bahati mbaya tu. Ningependa kukuhakikishia mtukufu mfalme kuwa, tunakuunga mkono kwenye jambo hili la ukeketaji.

MFALME MATATA: Watu wangu, wakati utakapofika kwa kiwavi kuwa kipepeo, hakuna mtu, hata kiwavi mwenyewe anaweza kufanya chochote. Kama walinzi wa

tamaduni, tutazingatia mila zetu. Kwa hivyo sherehe lazima iendelee kama inavyokuwa siku zote. Nenda mkatumikie watu wangu.

***** **MZIKI*******

MSIMULIZI: Ni usiku na katika sehemu moja ya Ufalme.Nyota na baba yake wanahusika katika hoja kali juu ya yeye kuhudhuria sherehe hiyo siku inayofuata.Kwa kuhisi kutokueleweka, anajielekea kitandani mapema. Amechanganyikiwa na yuko katika wingu la mawazo.

ONYESHO LA PILI

***** **MZIKI*******

MSIMULIZI: Jua linachomoza kwa sauti za shangwe katika Ufalme wa Kwetu, umande unang'aa juu ya nyasi wakati nyota anatoka ndani ya nyumba. Baba yake ameketi juu ya mwamba unaoelekea jua. Nyota ni miongoni mwa wasichana barobarowaloongea dhidi ya ukeketaji na masuala mengine ya kijamii ambayo yamekuwa kizingiti dhidi ya uendelevu wa wanawake wa ufalme wa KIKWETU. Pia ni miongoni mwa wasichana barobaro ambao wanafaa kukeketwa msimu huu, majibizano makali yanatokea kati yake na babake.

SFX SHANGWE NA NDEREMO

BABA NYOTA: Nyota, Nyota, tafadhali niletee kikombe cha chai
(Nyota anammiminia babake kikombe cha chai.)

BABA NYOTA: Kwa nini umekunja uso Binti yangu, ni asubuhi angavu na je unajua leo ni siku gani?

NYOTA: (*Akitizama chini*) Baba, nina woga, sidhani kama niko tayari kwa...

BABA NYOTA: Niskilize Nyota, sitaki kulizungumzia jambo hili tena.

Nyota: Baba tafadhali nisikilize, sisi kama wasichana na wanawake kutoka kijiji hichi hatujakubaliwa kutoa maoni yetu kuhusu yale mauchungu tunayopitia kutokana na tamaduni.

Baba Nyota: Sitarudia hili tena, na sitaki kuwa na mazungumzo zaidi, nenda ndani na ujitayarisha

***** **MZIKI*******

ONYESHO LA TATU

SFX SAUTI ZA USULI ZA NYUMANYUMA

MSIMULIZI: Wakati umefika na wasichana waliochaguliwa wanapelekwa katika nyumba maalum tayari kwa sherehe.

Mzee Tamaa anawasili nyumbani mwa baba Nyota kumchukua Nyota

MZEE TAMAA: Habari baba Nyota, kipepeo wangu yuko tayari?

BABA NYOTA: (Kwa sauti iliyo na shaka) Mzuri, oh ndio kweli! Labda yupo njiani akija.

MZEE TAMAA: Aha! Wacha niseme nimefurahi kukuhakikishia ng'ombe wote wako tayari na kama sehemu ya makubaliano yetu, nimeleta ng'ombe watatu hapa. Utawapata wengine wote baada ya masaa ishirini na manne. Umefanya kazi nzuri sana ya kumlea binti yako Nyota. Nitakuwa na furaha sana baada ya sherehe hizi kutamatika.

***** MZIKI*****

ONYESHO LA NNE

***** MZIKI*****

SIMULIZI: Nyota amekimbia nyumbani kwao. Amekaa kwenye mwamba akiangalia Ufalme wa Kwetu uliochini na kutafakari.

NYOTA: (*Akishangaa*) (Akijisemea kwa sauti) "Kwa nini watu wetu wako hivi? Ninaelewa njia zetu; walakini, sikubaliani na ukeketaji. Natamani watu wa kwetu wangeweza kukaa chini pamoja na kusikiliza kila mmoja. Nimepoteza marafiki zangu wengi kupitia ukeketaji na sasa wasichana wapatao 20 wataacha masomo kwa sababu sote tunatarajiwa kuolewa baada ya kukeketwa. Inaonekana ulimwengu wote umetugeuka. Mama ungalikuwa hapa ... Ni nani atakayenisikiliza? Ni nani atakayetusikiliza?"

***** MZIKI*****

WAHUSIKA: BI FARAJA, MZEE MAMBO, BABA NYOTA, MZEE BUSARA, MZEE 1

******* MZIKI *******

SIMULIZI: Ni wiki tatu baada ya tamati ya sherehe ya tohara, Bi Faraja ameandaa mkutano kwa watu wa Kwetu kujadili matukio ambayo yametokea kwenye utawala wa kifalme tangu sherehe. Bw. Mambo, Babake Nyote na mzee Busara wako pia, Umati unaonekana kuwa na furaha ila nyuso zao zinaonyesha ishara mchanganyiko. Kwenye kijiji kizima, Bi Faraja amekuwa makini kwa kusikiliza sauti za wasichana barobaro na wanawake waliopangwa kukeketwa kinyume na hiari yao. (Baadhi ya wazee walikuwawalikuwa wamekubali kuhudhuria mkutano ilhali wengine walimkinanai Bi Faraja kama mtu ambaye hangeweza kuwaita)

MZEE 1: Salamu watu wa Ufalme wa Kwetu. Nimefurahi kuwaona nyote mu wazima siku hii nzuri. Ninajivunia kuwa nyinyi nyote mmekumbatia na kuthamini utamaduni wetu. Roho za mababu zetu zinajivunia. Heshima kwa Mfalme Matata!

UMATI WA WATU: YEBA!!!!

MZEE1: Heshima kwa Mfalme matata!

UMATI WA WATU: YEZA!!!!

BI.FARAJA: Watu wa Kwetu, nawasalimu nyote. Ni kwa furaha kubwa kwamba nimesimama mbele yenu, kuwashukuru kwa ushirikiano wenu wa dhati wakati wa sherehe ya mpito. Wavulana wetu wamebadilika kuwa wanaume na sasa wanaweza kuulinda Ufalme wetu dhidi ya maadui zetu. Hata hivyo, ninamasikitiko makubwa sana ninapowaambia watu wangu kuwa wasichana wetu wawili wamepoteza maisha yao, na watano bado wanavuja damu hadi waleo na mmoja hajapatikana. Wengine wao itabidi waache shule na wafuate hatua ya kuolewa kama utamaduni wetu unavyolazimu. Tuna utamaduni mzuri ambao sisi sote tunapaswa kuulinda, lakini tunapaswa kukumbuka kuwa kama vile tunavyoridhia mti uliopandwa katika boma hutoa kivul cha kuvutia na matunda, iwapo matawi yake ambayo yatagusa paa ya nyumba yetu yanapaswa kukatwa.

MZEE MAMBO: Watu wazuri wa Kwetu, pokeeni salamu zangu, nahisi kuwa Bi Faraja yuko sabamba na maroho za mababu zetu. Anayasikiliza masilahi ya wasichana na wanawake na amesimama imara kuongea kwa pamoja kuhusu sauti za wasichana na wanawake wasiyo na sauti. Tumewapoteza wasichana wawili. Watano wangali wanavuja damu na kuudhihiri ubaya, elimu yao katika siku za usoni imekatizwa, watawezaje kushindana katika ulimwengu huu unaoendelea kukua, iwapo tungekuwa na wakati wa kuketi na kuyasikiliza masaibu ya wasichana wetu barobaro, tungeweza kuwa na uelewa wana uakaso kwenye machozi yao na udini kwenye sauti zao za ndani.

Mzee 1: Wazee wenzangu imitimia wakati wa kupea kipaumbelea malalamishi yaliyotolewa na wasichana na kinamama wetu kuhusu madhara ya ukeketaji na utamaduni wetu kwa maisha yao na katika elimu yao, vile vile kusababisha kiwewe ya kimwili na hata kifo.

Ni hali ya kusikitika kuskia kwamba tumepoteza mmoja wa wasichana wetu bila sisi kufahamu nini kilijiri, natumai ni wakati ya kuzungumzia swala kama wenyeji na kuleta njia mbadala. Mzee Busara

(YEBA! YEZA!YEBA!YEZA EE EE KWETU)*2

Watu wa Kwetu, Sasa nina furaha kwamba mawingu yanaliweka juu huru. Tazama! Hamuoni? Lazima tumfanye mfalme asikilize sauti za hawa wanawake barobaro. Naomba Bi faraja kuagiza kikao na mfalme ili tuwe na mkutano na watu pale Mwavulini na uhudhuriwe na barobaro kwa wazee.

SIMULIZI: Baba Nyota anasimama baada ya hotuba ya Mzee Busara huku kukiwa na manung'uniko ya umati. Bi Faraja anaahirisha mkutano na kila mtu anaondoka.

ONYESHO LA PILI

SIMULIZI: Baba Nyota ameketi kwenye mwamba kando ya Mto Kwetu. Mgurumo mzito wa mto unaoelekea katika nyanda za chini. Baba Nyota ako kwenya mawazo mazito huku akijizungumzia.

BABA NYOTA: Roho za mababu zetu, mbona mimi?! Lo! Ni kwanini mashaka haya yote yaliyounganishwa na ukeketaji huanzia na kumalizia na mimi? Ninalokovu ambalo halijawahi kupona moyoni mwangu. Kwanza alikuwa ni mke wangu. Alipoteza maisha

yake wakati akijifungua Nyota. Sijawahi kupata kazi ya kutunza familia yangu. Nilidhani kuwa ng'ombe 27 kutoka kwa Mzee Tamaa wangekuwa mafanikio kwa familia yangu. Lakini angalia sasa, mumemwondoa Nyota kutoka kwangu. Nifanye nini ili niwafurahishe nyinyi roho za ardhi yetu? Ondoeni laana katika familia yangu! Masikio yangu yako wazi kusikiza na kufanya lolote mtakalo, na moyo wangu uko tayari pia.

Ni muda tangu mwanangu alipotoweka na sijaskia kutoka kwa mwanangu nyota na sijui mahali alikokwenda.

Nitaanza kumtafuta wapi? Hakika nilimfanyia ubaya binti yangu na marehemu mke wangu, ROHO YAKO IPUMZIKE KWA AMANI MAMA NYOTA, laiti ningesikia vilio vyenu

Nina

uchungu sana kwa yale mliyoyapitia mioyo yenu pamoja na wanawake wengine.

Kuanzi leo nitapigania kutetea maslahi kwenye tamaduni zetu, tulikataa kuskiliza sauti zenu lakini sasa zinasikika zaidi kuliko hapo awali, nimefunguka macho na moyo wangu uko tayari kumsikiliza binti yangu, nimeanza kuona athari za ukeketaji, elimu, furaha, ooh binti yangu kwa nini sikuelewa athari za mila yetu.

Nirudie binti yangu, laiti ningelijua hili lingetokea

*****MZIKI*****

ONYESHO 3

SIMULIZI: Baba Nyota anaondoka kutoka ukingoni mwa mto na kuelekea kwenye boma ya Mzee Mambo pia. Anampata mzee Mambo na Mzee Busara wakiwa wameketi chini ya mti. Kwetu huku akielekea upande waliokuwa wamekaa. Anawakuta (BW. Mambo na mzee Busara) wameketi chini ya mti.

MZEE MAMBO: Ooh! Baba Nyota nimefurahi kukuona. Tulikuwa tunashauriana na mzee Busara kabla haujaingia. Umekuwa wapi?

BABA NYOTA: Ahsante sana BW. Mambo kwa kujali kwako. Leo kwenye mkutano, maneno yako ya busara na yale ya Mzee Busara kweli yalinigusa sana moyo wangu. Nahisi kama sauti ya binti yangu Nyotana wasichana wengine zinanitumia ujumbe. Kwa upole niongozeni kwa upole kwenye hali hii tatanishi, enyi wazee wenye busara wa nchi yetu.

MZEE BUSARA: Vizuri sana Baba Nyota, nahisi vivyo hivyo juu ya suala lako. Miungu inazungumza. Ninaelewa hisia ya kupoteza mbegu pasi kuiona ikinawiri! Ninaamini ila, kwamba mbegu hiyo imetua kwenye mchanga wenye rutuba na kuwa itamea na kuwa mti ambao utatoa kivuli kwa watu wake.

BABA NYOTA: Ninaelewa maneno yako Mzee Busara lakini nina hisia kuwa yamebeba maana nzito zaidi. Tafadhali nielezee kama mtoto mdogo.

MZEE MAMBO: Jambo ambalo Mzee Busara anajaribu kusema ni kwamba nilimuokoa binti yako Nyota alipokuwa anatoroka kutoka nyumbani. Alikuwa amechanganyikiwa na kuogopea mustakabali wake wa maisha ya baadaye baada ya kukeketwa. Kuna matumaini makubwa kwa binti yako Nyota. Macho yake yanaonyesha wazi. Niruhusu baba Nyota nimwangazie nuru yake. Nitamuelimisha.

SIMULIZI: Baba Nyota, akishangaa, akipiga magoti na kuinua mikono yake kuelekea angani. Furaha na buraha ingeweza kuonekana kwenye macho yake yaliyofurika machozi.

**** MZIKI****

SEHEMU YA TATU

ONYESHO LA KWANZA

**WAHUSIKA: MZEE MAMBO, BABA NYOTA, BI FARAJA, MAUA,
BW. BUSARA**

***** MUZIKI *****

SIMULIZI:Huku wakielekea nyumbani BW. Mambo anamueleza Baba Nyota kuhusu mkutano uliopangwa na Bi Faraja, na anamuomba waandamane naye.

Siku iliyofuata Bi faraja, Bwana Mambo pamoja na Baba Nyota wameketi pamoja sebuleni mwa Bi faraja. Katika sehemu hii, tunaye Bi Faraja, BW. Mambo na mkewe Bi Tamara, Baba Nyota, Maua na Bi Busara

Bi FARAJA: Habari ya Asubuhi mabwana?

MZEE MAMBO: Njema Bi Faraja, Kutana naye Rafiki yangu Baba Nyota, tulionelea vyema kukutana nawe juu ya mazungumzo yetu ya awali.

BI FARAJA: Karibu Baba Nyota.

BABA NYOTA: Ahsante Bi. Faraja.Ni fahari Yangu kukutana nawe.

MZEE MAMBO: Tumegundua kuna giza katika jamii yetu ambayo imetenganisha nguzo zinazoiweka jamii pamoja.

BI FARAJA: Naam, Nieleze zaidi.

MZEE MAMBO: Watu wetu wanaangamia kwa sababu ya kukosa maarifa. Ufalme wa Kwetu unavuja damu kwa kushikilia vipengee vya aambazo tumekataa kuziacha. Hata baada ya kuona madhara yake chanya kwetu.

BI FARAJA: Nafurahi kuwapata watu walio na maslahi mema mioyoni mwao kwa jamii yetu, inahitaji umoja kupigania mabadiliko katika jamii.

MZEE MAMBO: Tutawajibika kwa kizazi kijacho iwapo hatutawazia mabadiliko, ni sawa kufanya jambo la busara, Bi. Faraja, nyakati zimebadilika zimepita siku ambazo sauti za wanawake hasikuwa zinasikika ni wakati sasa wa kuskiliza wasichana na wanawake, na lazima tuwape nafasi ya kusiklizwa na zaidi ya hayo lazima tukumbuke hatari ya kisaikolojia na kimwili kuhusu ukeketaji.

BI FARAJA: Nakubaliana na wewe, nimejaribu sana kama naibu chifu, lakini sauti yangu

imezama kila wakati katikati ya upinzani, ninafuraha kuwa nimepata watu wanao kauli sawa na walio tayari kupanga njia mpya, kwa hivyo waungwana mnapendekeza hatua gani

MZEE MAMBO: Ningependa tusingitize umuhimu wa elimu kwa jamii kama chombo cha kuleta uhamasishaji na kuleta maendeleo katika jamii ili tuweze kufurahia matunda ya ufalme wa Kwetu. Elimu ni ufunguo na maarifa nguvu.

BI FARAJA: Baba Nyota maoni yako ni yapi?

BABA NYOTA: Kile ninachotaka ni kuona kwamba ukeketaji umetiwa kikomo, na wasichana wetu wameondolewa kwa mateso ya kimwili na kimawazo. Hebu wasichana wetu waafikie uwezo wao na haki zao kuheshimiwa.

BI FARAJA: vyema wangwana, nimewasikiliza na kutilia maanani maoni yenu. Mabadiliko ni majukumu yetu ni kutekeleza mabadiliko katika jamii. Nitaibua swala hili kwenye mkutano ujao kwenye Kasri.

MZEE MAMBO: Ahsante kwa kutusikiliza, tunaimani utawasilisha sauti za jamii yetu. Lakini ni muhimu sana tukiungana na wasichana na wanawake pamoja na wavulana na wanaume ili kujadili hatua za kusonga mbele na kusikiliza sauti ya jamii nzima ili tufanye kazi kwa pamoja.

(Mzee mambo na baba Nyota wanaondoka kuelekea Mwavuliini)

***** MZIKI*****

ONYESHO LA PILI

Mwavulini - Mzee mambo na Baba wanampata Mzee Busara akiwasubiri.

***** MZIKI *****

MZEE MAMBO: Ahh, mzee busara. Karibu sana. Sikuwa nikikutarajia.

MZEE BUSARA: Ahsante Mzee mambo, nina jambo la dharura ambalo linahitaji muingilio wako maramoja. Huyu hapa ni Maua.

MZEE MAMBO: Karibu Mwavulini Maua.

MAUA: Asante

MZEE BUSARA: Maua alikuwa mmoja wa wale wasichana ishirini waliokeketwa. Ila amekuwa akikumbwa na msongo wa mawazo kutokana na kile alichokipitia alipokeketwa. Ndiposa nikaonelea ni vyema nimlete huku ikizingatiwa kuwa una ujuzi wa kushughulikia maswala haya.

MZEE MAMBO: Oooh! nasikitika sana kusikia haya, Maua Karibu Mwavulini. Humu tunawasichana wengi wenye matatizo sawia na yako.

TAMARA: Usiogope Maua, hapa Mwavulini tutaendelea nawe kwa upendo, tutapitia haya pamoja kwa upendo na utunzi. karibu nyumbani.

*******MZIKI*******

SEHEMU YA NNE

ONYESHO LA KWANZA

WAHUSIKA: MFALME MATATA, CHIFU TUMBO MBELE, BI FARAJA, BI KIZEE, CHIFU 1, NYOTA,

****MZIKI****

SIMULIZI : Ni Baada ya miaka mitano nyota anarejea katika kijiji cha Kwetu akiwa amemekomaa na mwenye maarifa zaidi baada yakupata elimu, anajaribu kurekebisha tabia, mila na desturi zenye madhara katika jamii ya Kwetu. Kulingana na upelelezi wa nyota wasichana katika kijiji hiki bado wanakeketwa, kutoendelea na masomo na kuozwa mapema. Na sasa yuko tayari kukutana na mfalme wa kijiji cha Kwetu.

Ndani la kasri Mfalme Matata amewaita mkutanoni machifu, manaibu wa chifu, wazee wa kijiji na Bi. Kizee. Naibu wa chief Bi. Faraja anakashifiwa kwa kuendelea kupinga baadhi ya tamaduni za ufalme.

MFALME MATATA: YEBA Kwetu kingdom! Yeba yeba viongozi wa Kwetu!

Ummati: Yeza yeza mfalme wa kwetu

MFALME MATATA: Nimewaita nyinyi wote leo hii kuwakumbusha kuhusu mila, desturi na majukumu ambayo kila mmoja anafaa kushikilia. Ningependa kuwapongeza baadhi yenu ambao wamejitolea kwa uendelevu wa ufalme wetu. Imenijia kuwa baadhi yenu wanania kuisambaratisha falme yetu. Bi faraja si mara moja si mara mbili nimepokea malalamishi kwamba unaenda kinyume na tamaduni zetu...hebu simama mara moja!

CHIFU TUMBO MBELE: Nilijua! Nilijua! Mfalme nimekua nikikueleza mara kwa mara huyu ndiye ambaye amekuwa mwiba wa ufalme huu.

(sauti ya wananchi wakimzomea)

BI FARAJA: Lakini..... lakini

MFALME MATATA: Kimya

*****MZIKI*****

ONYESHO LA PILI

*****MZIKI*****

SIMULIZI: Katika hali ya mchanganyiko huo, kila mmoja ana nyamaza na kumwelekezea macho kwa mshangao Nyota ambaye anatembea akielekea mbele ya mfalme

BI. KIZEE: Nakukumbuka, wewe ndiye uliyetoroka wakati wa sherehe miaka kadha iliyopita. Ujaribuje basi kuonyesha uso wako hapa?

CHIFU 1: Huwezi kurudi hapa!

MFALME MATATA: Nyamazeni yeye ni nani?

CHIFU TUMBO MBELE: Yeye ni. (Nyota anaingilia)

NYOTA: (Anaingilia) Mimi ni Nyota binti wa ardhi hii, Niliondoka kutoka falme hii miaka 5 iliyopita nikitorokea ukeketaji. Sasa nina maarifa na busara zaidi. Mfalme, kwa hiari yako naomba unisikize.

MFALME MATATA: Kuhusu nini?

NYOTA: Mfalme, kwa kuwasikiliza watu utapata uwaminifu wao na kwa pamoja wataweza kujua mabadiliko muhimu yanayofanyika katika maisha yao na jinsi wanavyohisina uhusiano na mabadiliko hayo. (kimya)

MFALME MATATA: Askari, mpeleke kwenye kasri langu.

NYOTA: Hapana mfalme naomba nikasikizwe na kila mmoja.

ONYESHO LA TATU

SIMULIZI: Nyota alivyokataa kufuata maelekezo ya ya mfalme Matata, Mfalme anaondoka kwenda kwa kasiri na kurudi. Anashtuka kwa ujasiri na ukakamavu ulio kwenye macho ya nyota.

MFALME MATATA; Naam Nyota, sasa nakupa fursa. Ni lipi ungetaka kumwambia mfalme wako?

NYOTA: Mfalme, nilitoroka kwa sababu hakuna aliyetaka kunisikiliza, ndoto za wasichana wengi barobaro zimedhuriwa kwa jina la tamaduni na mila zetu. Niliogopa iwapo ningeketwa ningefariki na iwapo ningeponea ningelewa na ndoto yangu ya kupata elimu na kurejesha mkono wa heri kwa jamii kusambaratishwa.

MFALME MATATA: Kwa nini unaniambia haya yote?

NYOTA: Nimejifundisha kuhusu mbinu ya PFIM ambayo inayohusisha kuskiliza sauti ya jamii na kuonyesha huruma ili hekima na uelewa wa watu upate kuheshimiwa.

Mfalme wangu ni muhimu kuwasikiliza wasichana na wanawake wetu na kuwashirikisha katika masuala na maamuzi yanayohusiana na maisha yao.

MFALME MATATA: Mbona nifanye hiVyo?

NYOTA: Mfalme tukielezana ukweli kama kila mmoja wetu tutaruhusu uelewano wa pamoja na umiliki wa pamoja wa kuendeleza ufalme wetu mbele.

MFALME MATATA: Ni umuhimu gani utakaoleta katika Jamii ya Kwetu??

NYOTA: Iwapo kila kila maoni ya wanajamii yatasikilizwa , tutakuwa na sauti sawia ambayo itatusaidia kuiboresha jamii. Mtukufu mfalme, jamii yenye furaha ni jamii yenye afya, na wewe mfalme mpendwa utuongoze kwa hekima

MFALME MATATA: Wow! Nyota ama kweli umebadilisha mtizamo wa fikira zangu. Ni busara ya aina gani hii? Ningependa kujua zaidi. Tunaweza kupanga mkutano?

NYOTA: Ndio mfalme wangu!

SIMULIZI: Baada ya mkutano na Nyota, mfalme anawaamuru machifu kuwahamasisha watu kukutana kwa siku chache Mwavulini pahala pa kawaida pa mikutano.

****MZIKI****

SEHEMU YA TANO

ONYESHO LA KWANZA

WAHUSIKA: MAMA 1, MAMA 2, BI FARAJA, MAMA TUMAINI, MFALME MATATA, MZEE BUSARA, MZEE TAMAA, HABIBI, NYOTA

*****MZIKI*****

SIMULIZI.: Ni siku chache zimepita baada ya mkutano uliohudhuriwa Mfalme Matata Nyota kwenye Kasri na mkutano mwingine wa jamii unaandaliwa pale Mwavulini.

MAMA 1: Hey! Mbona una haraka hivyo?

MAMA 2: Nakimbia nikielekea Mwavulini

MAMA 1: Mwavulini? Mwavulini, kuna nini?

MAMA 2: Kwani haukuwa sokoni jana? Ilitangazwa kuwa tutakuwata na Mfalme atakuwepo. Hata hivyo nashuku kama atakuja. Mfalme na baraza lake kila wakati hutupa habari lakini huwa hasikilizi sauti zetu

MAMA 1: Ahh! Mfalme? Agenda yako ni gani? Yote hayo, ni taratibu tu. Wazee na mfalme wanakuja kila wakati na ajenda na huwa hawasikii sauti zetu.

MAMA 2: Labda ndiyo, Lakini ingali ni wajibu wetu kuhudhuria mkutano kama hiyo.

MAMA 1: Kwa nini tuhudhurie wakati maamuzi yote ya jamii hufanywa kwa niaba yetu? Kutakuwa na chochote chetu?

MAMA 2: Bi Faraja ndiye aliyeupanga na kuitisha, na labda mfalme atahusika. Naamini ni wazo nzuri kuhudhuria..

MAMA 1: Naam, ninamuamini Bi. Faraja. Nitaenda sokoni baadaye; hii ni muhimu Zaidi.

Simulizi: Baada ya muda mfupi, mama 1 na mama 2 wanawasili Mwavulini, Kuna manung'uniko, watu wana wasiwasi na wanashangaa mfalme anafanya nini miongoni mwao.

BI FARAJA: Habari za asubuhi mabibi na mabwana,? Asanteni kwa kuja kwenye mkutano huu. Leo tumekuja kuwasikiliza.

Simulizi: Baada ya utangulizi, majadiliano juu ya sababu ya mkutano yanafuata.

BI FARAJA: Tafadhari kututaarifu kwa pamoja mambo muhimu ambayo yamekuwa yakifanyika katika maisha yenu miaka michache iliyopita.

MAMA TUMAINI: Asante kwa kuita mkutano huu. Hata hivyo hatufahamu kwa uhakika ajenda ya mkutano huu.

Hello, Watu wangu, ahsante kwa swali lako Bi. Tumaini. Leo hii tumekusanyika hapa ili kushiriki na kuelewa jinsi mnavyohisi juu ya mambo muhimu kwenu na jinsi tunaweza kufanya kazi kwa ushirikiano. Tuko hapa kusikiliza kila mmoja kama mandugu na madada wanaoishi katika Ufalme wa Kwetu

MZEE BUSARA: Nataka kushukuru kwa fursa hii, kwa kuwa hatujawahi kuwa na mkutano wa wazi hapo awali. Mambo mengi yametokea katika ufalme huu. Tumekuwa na mvua nzuri na mavuno ya fadhila katika miaka iliyopita. Sherehe ilikuwa tu hivi majuzi, ambapo tulikumbatia utamaduni wetu.

(Anaketi)

BI FARAJA: Asante kwa kushiriki mzee Busara. Nani angependa kuzungumza wa kwanza?

MZEE TAMAA: Asante kwa fursa hii. Kwa kweli, mimi nina huzuni kwa sababu hivi majuzi nilimpoteza mke wangu. Nilidhani ni kifo cha kawaida lakini sasa naelewa ni kwa sababu ya sehemu moja ya tamaduni yetu. Nafikiri kukeketwa ni hatari. Natamani tungekuwa na njia mbadala ya kuwawezesha wasichana wetu kufuzu kutoka ujana hadi utuuzima. Asanteni.

MAMA TUMAINI: Asante kwa kushiriki mzee tamaa na pole kwa kumpoteza mkeo. Mimi mwenyewe nilipitia ukeketaji miaka michache iliyopita na kwa sababu hiyo, nikapata shida. Sasa natatizika sana kudhibiti kwenda haja ndogo na kubwa. Hii ilikuwa ni baada ya mimi kupata mpasuko nikijifungua mwanangu wa kiume. Kutokana na uchungu wa mwana wa muda mrefu, mwanangu Tumaini alizaliwa akiwa na changamoto za kiakili.
(Hisia na hisia zinafufuliwa)

MAMA TUMAINI: Natamani jamii yangu ingenikubali mie na mwanangu, Ninahisi upweke, Watu hapa kama mlaanifu wa jami. Wanafikiri mimi ni mchawi. Hi hunifanya kuhisi mimi si mmoja wao. Natamani ingekuwa na uelewa zaidi. Naheshimu tamaduni zetu, lakini singependa kuona msichana yeyoyote katika jamii yetu akipitia niliyoyapitia.

Baada ya Nyota kuchangia, kuna manung'uniko machache.

Asante mama Tumaini kwa kuzungumza. Ningependa kuhadithia yaliyonikumba miaka michache iliyopita. Nilitoroka nyumbani kwetu miaka michache iliyopita kuepuka ukeketaji,kuolewa kwa mapema na ari yangu ya kupata elimu njia ambayo ningeweza kuisaidia jamii yangu. Nilipata hifadhi salama Mwavulini. Ningependa kumshukuru Bw. Mambo kwa kunisaidia mimi na wasichana wengine. Niilikuwa nimefikiri kupanga mkutano kama huu wakati huo, lakini nina furaha kuona unafanyika sasa.Kwa kusikilizana kila mmoja, tunaweza sote kuthamini uwezo wetu, fursa na maarifa na kuzindua njia bora za kudumisha utamaduni wetu bila kupoteza matumaini na maisha.

Mfalme Matata: Asante kwa kushiriki Nyota. Nakubaliana nawe. Hebu tuzidi kuelezea tuliyoyapitia.

HABIBI: Kwa upande wangu, napenda kumshukuru Bi. Faraja kwa nafasi hii ya watu wetu kushirikisha maoni yao. Tofauti na Nyota aliyepuka ukeketaji,yangu niliopitia ni ya uchungu mwingi katika maisha yangu. Nikiwa Mwavulini niliweza kupata usaidizi wa kimatibabu,pia nilipata motto na nililikuwa hali moja na mama Tumaini.

MAMA TUMAINI: Asante kwa kushiriki. Sasa ninahisi nina matumaini kuwa naweza kupata msaada.

MAMA 2: Kuleta jamii pamoja kumekuwa na faida kubwa. Sijawahi kuhisi kuwa wazi kuzungumzia maoni yangu ambapo yamesikilizwa na kuheshimiwa. kupitia kutushirikisha tumeweza kusikilizana. Kama jamii tunaweza kutoa msaada kwa akina baba pweke kama vile Mzee Tamaa na mtoto wake. Pia nina binamu yangu ambaye angefaidika sana na huduma za Mwavulini.

MFALME MATATA: Leo tumesikiliza kwa makini masuala mlioibua, changamoto kama vile ukeketaji, mvua nzuri na mavuno mema na pia nyumba inayosaidia wanawake wenye matatizo, naomba tuendelee kukutana ili tuweze kujadiliana na kushirikiana kwa mawazo ili kupata suluhu ya kusaidia watu wetu na jinsi tunavyoweza kuendeleza tamaduni salama za mpwito kwa wasichana wetu wadogo ya kuwaheshimu na kuheshimu tamaduni zetu.

Imekuwa heshima kubwa ya kuwasikiliza nyinyi nyote. Kwa kweli lazima nikiri kuwa kuna mengi ambayo sikuyajua na nimejifunza kuwa kuwaweka mbele kwanza tunaweza kufanya kazi pamoja. Pia nimejifunza kusikiliza, na kuheshimu maoni ya kila mmoja. Naamini kuwa hili litanifanya kuwa kiongozi bora.

MFALME MATATA: YEBA ufalme wa kwetu!!

ummati: YezaYeza Ufalme wa Kwetu!

(mziki)

YEBA YEZA, YEBA YEZA

EE EEH KWETU! X 2

*******MZIKI ******

*******MWISHO*******



Umoja Radio For Peace



Kenya Community
Media Network
(KCOMNET)



german
cooperation

DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

giz

Deutsche Gesellschaft
für Internationale
Zusammenarbeit (GIZ) GmbH



20 Jahre
Deutsche Gesellschaft
für Internationale
Zusammenarbeit (GIZ) GmbH
We don't just see borders, we see them.

Kenya Community Media Network

Shalom House, off Ngong Road, St. Daniel Comboni Rd, Wing C, 1st Floor

P.O Box 2641 - 00100, Nairobi | Tel: +254 725 262 623

www.umojaradioforpeace.org

www.sikika.net